**SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA**

**(SURA YA 290)**

---

**SHERIA NDOGO**

---

***(Zimetungwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16(1)***

# SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA NYUMBA ZA KULALA WAGENI) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA TANDAHIMBA ZA MWAKA 2023

*Jina na mwanzo wa kutumika*

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Ushuru wa Nyumba za Kulala Wageni) za Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba za mwaka 2023 na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

*Matumizi*

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba.

*Tafsiri*

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:-

**"Afisa Mwidhiniwa"** maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;"

**"Daftari la Wageni"** maana yake ni kitabu Maalumu kilichoandaliwa na Mmiliki au kilicho nunuliwa kwa lengo la kusajili na kutunza kumbukumbu za wageni wanaolala kwenye nyumba ya kulala wageni au hoteli.

**"Gharama ya malazi"** maana yake ni kiasi cha fedha kinachotozwa na mmiliki wa nyumba ya kulala wageni kwa mtu ambaye anapata huduma ya malazi.

**"Hoteli"** maana yake ni jengo lililojengwa kwa ajili ya kupokea na kulaza wageni kwa lengo la kupata faida na haitajumuisha jengo lenye vyumba chini ya 6, lakini pia haitajumuisha Mabweni na Nyumba za mapumziko za Serikali"

**"Mkurugenzi"** maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba au Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza kazi za Mkurugenzi chini ya Sheria Ndogo hizi;

**"Mgeni"** maana yake ni mtu yeyote ambaye hulipa pango la kukaa kwenye chumba cha kulala wageni, aidha kwa siku nzima au sehemu ya siku nzima;

**"Mmiliki"** maana yake ni mtu yeyote anayemiliki kihalali nyumba ya kulala wageni au hoteli na inajumuisha mtu yeyote aliyepewa na mmiliki, jukumu la kusimamia Nyumba ya kulala Wageni au Hoteli au mwajiriwa au mtu yeyote anayehusika kukusanya gharama za pango toka kwa mgeni kutokana na mgeni huyo kulala kwenye nyumba hiyo ya kulala wageni;

**"Nyumba ya kulala Wageni"** maana yake ni jengo lililojengwa kwa ajili ya wageni kwa lengo la kupata faida ambayo itajumuisha jengo ambalo lina vyumba vya kulala wageni visivyopungua 6 vinavyotumika kutoa huduma ya vyumba vya kulala. Tafsiri hii haitajumuisha nyumba za mapumziko za serikali.

*Kiwango cha ushuru*

4. Kila mmiliki wa Hoteli au Mmiliki wa nyumba ya kulala Wageni/Hoteli atalazimika kulipa Ushuru wa nyumba za kulala wageni kwa Halmashauri, ushuru ambao utakuwa sawa na asilimia kumi (10%) ya mauzo ya siku kwa kila chumba au vyumba vyilivyolaza wageni.

*Uwezo wa Afisa Mwidhiniwa kukagua*

5. Afisa Mwidhiniwa atakuwa na wajibu wa:-

(1) kukagua nyumba ya kulala wageni/hoteli kwa lengo la kutaka kujua kama wageni wote wameingizwa kwenye daftari la wageni;

(2) kukagua kama mmiliki au mtunza nyumba ya kulala wageni/hoteli anacho kitabu cha wageni;

(3) kukagua nyumba ya kulala wageni/hoteli na kuhakikisha inafanyakazi iliyokusudiwa;

(4) kukagua kama mapato ambayo hulipwa Halmashauri yanaendana na hali halisi ya mapokezi ya wageni;

(5) kakagua kama nyumba ya kulala wageni ipo katika hali ya usafi;

(6) kukagua kama kwenye nyumba ya kulala wageni kuna mahitaji yote ya msingi na lazima yanayotakiwa kuwepo; na

(7) kukagua kama taratibu za kulaza wageni kwenye nyumba ya kulala wageni zinafuatwa.

*Masharti ya mmiliki /mtunza Hoteli*

**6.** Kila mmiliki au mtunza hoteli au nyumba ya kulala wageni atahakikisha yafuatayo yanatekelezwa/yanafanyika:-

(a) kila mgeni anasajiliwa kwenye daftari la wageni kwa kuingiza taarifa zake zote muhimu bila kujali muda aliokitumia chumba;

(b) kila kitanda hakitaruhusiwa kutumika na wageni wawili au zaidi wa jinsia moja;

(c) kulipa Ushuru wa nyumba ya kulala wageni/hoteli kwa Halmashauri ndani ya siku 7 baada ya mwezi husika wa mauzo;

(d) kulipa ada ya leseni ya biashara ya nyumba ya kulala wageni ndani ya muda uliowekwa kwa mujibu wa Sheria;

(e) kuhakikisha kuwa nyumba ya kulala wageni inakuwa safi muda wote na masharti mengine ya usafi yanafuatwa;

(f) kuweka wazi vitabu vya kumbukumbu za wageni na nyaraka zingine wakati wa ukaguzi;

(g) kuhakikisha kuwa biashara ya nyumba za kulala wageni/hoteli inakuwa na leseni itakayowekwa wazi katika eneo la biashara na kuzingatia masharti yote kama yalivyo fafanuliwa kwenye Sheria ya Leseni na miongozo ya biashara;

(h) Kutoa ushirikiano wa kutosha kwa Mkurugenzi, Afisa mwidhiniwa ikiwa ni pamoja na maafisa mbalimbali wa serikali wakati wote wa kufanyika kwa ukaguzi wa aina yoyote.

Wajibu wa mmiliki

**7.** Itakuwa ni jukumu la kila mmiliki au mtunza hoteli/nyumba ya kulala wageni kuhakikisha kuwa:-

(a) kunakuwa na ulinzi wa kutosha wa mgeni/wageni na mali zao na kuhakikisha kuwa milango na madirisha ya kila chumba ni imara;

(b) kwenye kila chumba cha kulala mgeni yanatolewa mahitaji yote ya msingi ambayo ni sabuni ya kuogea, mswaki, dawa ya meno, kondomu, maji ya moto, taulo, mashuka na mahitjai mengine

muhimu kwa mgeni/wageni;

(c) kutoa stakabadhi za kielektroniki kwa kila mgeni/wageni mara baada ya kupokea malipo;

*Kibali cha kuendesha biashara ya nyumba ya kulala wageni*

8. Kibali cha kuendesha biashara ya nyumba ya kulala wageni, kitatolewa baada ya Halmashauri kujiridhisha kuwa katika jengo hilo kuna:-

(1) mwanga na hewa ya kutosha;

(2) nafasi na vifaa (samani) za kutosha;

(3) mfumo wa uondoshaji wa maji taka na taka ngumu wa kuaminika;

(4) usafi wa jumla wa jengo na vifaa vyake;

(5) vyoo na mabafu kwa jinsia zote;

(6) vifaa vya zima moto;

(7) tanki la kuhifadhia maji safi;

(8) vyoo na bafu vilivyosakafiwa vema kwa vigae au marumaru na kuta zake ziwe zimewekwa vigae kiasi cha futi sita kutoka usawa wa sakafu;

(9) kuwa na jozi zaidi ya mbili za mashuka, foronya za mito na magodoro kwa kila kitanda na ziwe na rangi isiyoficha uchafu;

(10) kuwepo na sehemu maalumu ya kufulia na kuanikia nguo;

(11) stoo na chumba cha kubadilishia nguo kwa ajili ya wafanyakazi wa hoteli/nyumba husika ya kulala wageni;

Kosa

9. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa iwapo atafanya mambo yafuatayo:-

(a) atakuwa na vitabu vya wageni zaidi ya viwili;

(b) hatoandikisha jina au majina ya wageni waliolala kwenye hoteli/nyumba husika ya kulala wageni;

(c) atamzuia Afisa Mwidhiniwa kufanya ukaguzi katika nyumba ya kulala wageni au hoteli;

(d) atakiuka kipengele chochote cha sheria ndogo hizi

| | | |
|---|---|---|
| Adhabu | 10. | Mtu yeyote atakayekiuka au kwenda kinyume na kifungu chochote cha Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua Shilingi Laki Mbili (**200,000.00**) na isiyozidi Shilingi Milioni Moja **(1,000,000.00)** au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote faini na kifungo kwa pamoja. |
| Uwezo wa Mkurugenzi kufifilisha kosa | **11.** | Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiyari yake mwenyewe kwa maandishi kwa kujaza fomu maalum iliyoambatishwa kwenye **Jedwali** la Sheria Ndogo hizi na kulipa Ushuru anaodaiwa pamoja na faini ya shilingi Laki Mbili (**200,000.00**). |

**JEDWALI**

***(Limetungwa chini ya kifungu cha 11)***

**KUFIFILISHA KOSA**

Mimi…………………………………………. Nakiri, kwa hiari yangu mimi mwenyewe, mbele ya ……………………………………….……ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba, kwamba mnamo tarehe…………ya mwezi………..mwaka **20……..**nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha ………………………cha Sheria Ndogo za (Ushuru wa Nyumba za Kulala Wageni) za Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba za mwaka 2023.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba, kwa mujibu wa sheria, nipo tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe………….ya mwezi……………Mwaka 20……………..

Jina…………………………………..…..

Saini…………………………………..….

**Mbele ya:**
Jina………………………………………..
Cheo………………………………………
Saini……..………………………………..
Tarehe: ………………………………….

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba ilibandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa azimio lililopitishwa na Halmashauri katika kikao kilichoketi na kufanyika tarehe……………………… na ilibandikwa mbele ya:

…..………………………………
**Mussa Laurence Gama**
*Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba*

…………………………………
**Baisa Abdallah Baisa**
*Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba*

**NAKUBALI**

**……………………………………………………**
**ANGELLAH JASMINE KAIRUKI (MB)**
**WAZIRI WA NCHI – OFISI YA RAIS**
**(TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITA)**

**Dodoma,**
**Juni, 2023**